

# Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA  
KAZI YA KIMISHENI ULIMWENGUNI KOTE

## SAFISHA KWANZA

Yesu aliwatazama waandishi na Mafarisayo na kuwaonya: "Mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi . . . safisha kwanza ndani . . . ili nje yake nayo ipate kuwa safi. Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenyewe haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi" (Mathayo 23:25-28).

Mafarisayo walivaa mavazi yao kwa kusudi la kuonekana wenyewe haki na watakatifu machoni pa watu wale wengine. Lakini Yesu alifahamu miyo yao na kuwaambia "kusafisha kwanza" mtu wa ndani. Basi kilicho muhimu zaidi mbele zake Mungu hata kuliko aina ya nguo ambayo mtu anavaa ni hali yake ya moyo. Hata nyakati hizi zetu watu

wengine hufanya kama Mafarisayo wa hapo kale. Wao hutaka kuhesabiwa haki kwa matendo yao mema na mavazi yao ya wastani huku wakiwa na nia ya kutukuzwa na wanadamu kutokana na matendo yao mema. Lakini Yesu alifundisha kwamba sio mambo ya nje humnajisi mtu, mbali mtu hunajisiwa na "vitokavyo moyoni" (Mathayo 15:17-20). Kama moyo wa mtu haukulaliki machoni

pa Mungu viwango anavyodumisha maishani mwake na matendo yake yote yatakuwa bure. Mtu akidumisha viwango bora kwa mambo yanayookeana na wanadamu, lakini atumie jambo hilo kuficha hali yake ya kukosa utakatifu wa moyo, huo ni unafiki mtupu.

vyake nya mavazi vinatokana na moyo safi. Watu hawaokoki ama kuhesabiwa haki kutokona na kazi zao mbali kupitia kwa neema inayokuja kwetu kupitia kwa imani (Waefeso 2:8-9). Ni wakati moyo wa mtu umebadilishwa kwa nguvu za Yesu Kristo ndipo mtoto wa Mungu anahitajika kufuata utakatifu katika kila fani ya maisha yake; asipotafuta utakatifu huo yeye hatoweza kamwe kumwona Bwana wake (Waebrania 12:14).

Mtu akipata wokovu ambaa unaingia moyoni mwake yeye hubadilika sana, "Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi, na kufanywa watumwa wa Mungu, mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele" (Warumi 6:22). Dhambi, kiburi, tamaa, matendo ya kujivuna, n.k. hutakaswa na kung'olewa maishani mwake. Hii ndiyo sababu Waefeso 4:23-24 inasema, "Mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; na mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli."

Maandiko mengi hushughulikia sana swala la umuhimu wa mtu wa ndani kuwa safi kwa sababu wakati mienendo

(Inaendelea kutoka ukurasa 2)



SAFISA KILICHO  
NDANI  
KWANZA.

# MAMBO AMBAYO

# BIBLIA

## Inafundisha Kuhusu...

### Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

### Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, I Yoh. 4:7-21

### Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

### Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

### Uhuru Kutokana na Dhambi

I Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

### Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

### Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, I Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

### Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

### Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, I Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

### Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

### Kinuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

### Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

### Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

### Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

### Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

### Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

### Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

### Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa I)

ya mtu wa ndani inalingana na roho wa Kristo, tunda linaloonekana kwa nje na wanadamu wale wengine linakuwa tunda takatifu. Biblia nayo haineni kinaga-ubaga kuhusu kila sehemu ya maisha ya mwanadamu lakini inatoa kanuni ambazo mtu anahitaji kufuata ili aweze kumtukuza Mwenyezi Mungu. Mtu anahitaji kuamua atavaa au kutenda kwa njia gani kwa kufuata misingi ya kanuni za Biblia. Ingawa watu wa dunia hujaribu kutoa vijisababu ili kujihesabia haki kwa mambo wanayotenda, Roho wa Mungu atamwongoza kwa ukweli kila ambaye anatafuta ukweli kwa moyo safi.

Mungu wa Mbinguni hudumu ndani ya "yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekrea" (Isaya 57:15). Naye mtume Petro anawafundisha watoto wa Mungu kwa kuwaambia "jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wengine kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema" (1 Petro 5:5). Kulingana na jinsi moyo wa mwanadamu ulivyo mnyenyekevu machoni pa Mungu ndivyo mtu wa nje anayeonekana na wanadamu atahitaji kudhihirisha unyenyekevu huo wa ndani. Hii ndio sababu 1 Petro 3:4 inasema kwamba, "Bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu."

Utakatifu ni jambo linalofaa sana machoni pa Mungu. Yeye anahitaji kuabudiwa na kuonyeshwa heshima kuititia hekalu takatifu la mwili wa mwanadamu ambaye amejitoa kikamilifu kwake: "Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenye; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu" (1 Wakorintho 6:19-20).

—mws

### UKWELI WA INJILI

Gazeti la 'Ukweli wa Injili' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwashimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamiletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinasi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

### UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka jinsi mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) ili uagize jalida hili kuititia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

### WASILIANA NASI

Gazeti la Ukweli wa injili linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimisheni ambazo sisi hufanya huwezesha kuititia kwa matolea ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA

[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

# Tahariri



*Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu amba ni wetu sisi sote, nalionna imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. – Yuda 1:3*

Mzigo ulioko moyoni mwangu kwa robo (hii) ya mwaka ni kuhusu, "Jinsi Mkristo anavyoonekana kwa nje, au mavazi anayovaa Mkristo." Mungu angali anadumisha viwango nya jinsi ambavyo Mkristo anastahili kuva, hata ingawa Wakristo wengi hufuata viwango nya dunia katika jambo hili.

Lakini tofauti kati ya watu wa Mungu na watu wa dunia itazidi kuwa kubwa kulingana na jinsi ambavyo uovo utakavyoendelea kukidhiri katika siku hizi za mwisho. Ni ombi langu kwamba Bwana wetu atatusaidia kuendelea kupigania imani ambayo tulipiata kuitia kwa Neno lake. Nawe msomaji wangu, mimi ninakuhimiza uendelee kushikilia mafundisho yanayofaa ya Ukristo bila kutingisika. Kama kuna mambo ambayo wewe huelewi basi ninakuomba uwe mwangalifu sana ili usiondoe alama na mipaka ambayo iliwekwa hapo siku za kale, mipaka ambayo ingali yafaa hata wakati huu ambapo nyakati zimesonga sana.

Neema za Mungu ambazo zinafanya kazi ndani ya mwanadamu ni muhimu zaidi kuliko jinsi mtu wa nje anavyoonekana. Ni jambo la aibu kuona jinsi watu wanavyoendelea kujivunia kuva mavazi ya kiwango cha wastani huku tabia zao zikiwa za kimwili, zeny kiburi, na zilizokosa upendo. Lakini pia ni ukweli kwamba jinsi mtu anavyoonekana kwa nje ni sehemu ya maisha tunayoishi na Maandiko pia huzungumzia swala hilo. Kwa kweli mambo yote tunayofanya yanahitaji kulingana na uhusiano wetu na Mungu.

Wakati mwingi watu hawapendezwi wahubiri wakihubiri kuhusu jinsi mtu wa nje anavyostahili kuonekana, hasa wakati wachungaji wakisema moja kwa moja kuhusu jinsi ambavyo Mkristo anastahili kuva. Ni jambo la huzuni kubwa kuona kwamba hata watu wanaoamini haja ya utakatifu huona aibu kuzungumzia swala hili. Ingawa ni kweli kwamba mambo hayo yanahitaji kuzungumziwa kwa hekima, lakini hakuna wakati "unaofaa" kulizungumzia swala hilo. Je, watu watajifunza vipi kuhusu mipango ya Mungu ikiwa wahubiri hawatahubiri kuhusu mipango hiyo? Kulingana na jinsi ambavyo watu wengi kwenye makusanyiko yetu wanavyoishi kwa viwango duni nya maisha, ndivyo itakuwa vigumu kwa wachungaji kuhubiri kuhusiana na maswala hayo. Mambo mengine yanaonekana kuwa si muhimu, na hata wengine wanasesha hayo sio mambo ya kuangaziwa sana; lakini wakati watu wakianza kukosa kuwa na uangalifu na kuanza kufanya mambo kulingana na dunia, mwisho wake mara nyingi huwa ni kanisa kupatwa na janga la kiroho.

Mimi ninakumbuka sana kuhusu swala tata la tai ya shingoni ambalo lilikanganya sana dhehebu la Kanisa la Mungu. Mgawanyiko ulizuka katika mwaka wa 1910-1913 wakati ambapo kati ya maswala yaliyokuwa tata lilikuwa lile la uvaaji wa tai. Washirika wengine walikuwa tayari kukubali kwamba vazi hilo la kuzungukia shingo halikuwa na maana yoyote. Nao wengine walitilia mkazo jambo hilo ili maisha yao "yalingane" na jamii ya wakati huo. Basi hata ingawa tai lilikuwa vazi ndogo, wale waloliukubali waliacha kutilia maanani mambo mengine makubwa ya ukweli. Katika dhehebu hilo la kanisa la Mungu, kutoka wakati huo hadi sasa, hakujawahi kuwa na kiwango cha Biblia kilichokubalika kuhusu haja ya washirika kuva mavazi ya kiwango cha wastani. Basi ni jambo muhimu sisi kuangazia ukweli kuhusu swala hilo. Kulingana na mitindo ya kisasa, wanawake wa Marekani wanawenza kuva skafu nzito shingoni mwao kama mapambo. Basi ni kanuni gani inahitaji kufuatwa mtu anapoamua aidha kuva au kutovaa tai au mkufu shingoni? Kanuni, sababu, na roho ambayo inakufanya wewe kutenda jambo moja au nyingine ndio kitu muhimu zaidi kuliko vazi lenyewe.

Kwa kweli sisi hatungetaka tu kuunga mkono swala la kutilia sana haja ya mtu kufuata sheria, wala hatutaki kuwa na misimamo mikali kuhusiana na mambo hayo. Lengo letu hasa ni kuhimiza Mkristo kuishi maisha ya kiroho ambayo ina mizani inayofaa. Kuna uwezekano wa sisi Wakristo kuwa na tofauti ndogo ndogo kuhusu viwango vinavyohitaji kufuatwa na Wakristo kwa mambo ya jinsi mtu anahitaji kuonekana kwa nje, lakini mimi mwenyewe naonelea kwamba tofauti hizo hazitakuwa kubwa sana mradi sisi sote tutuafuata kanuni za Biblia ambazo ni dhahiri kabisa. Ni jambo la baraka kubwa mtu kuishi maisha ya unyenyekevu na yenye kudumisha viwango nya wastani ndani ya Yesu Kristo. Basi ni ombi letu kwamba Bwana Yesu atatupatia amani na ujasiri wa kusimama wima katika ukweli katika ulimwengu ambao una giza nyingi na tuweze kuishi maisha ambayo yanampendeza Bwana Mwokozi wetu.

Michael W. Smith

April 2016.

Mengi kwa  
MTANDA

**Tutembelee kwa**

[www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org)

**ili uagize na kusoma**

**jarida letu.**



## MAKARIBISHO

.....

Watu wa Mungu hukaribisha katika ibada zao watu amba mavazi yao hayalingani na kanuni za Biblia kuhusu jinsi Mkristo anastahili kuva mavazi ya kiwango cha wastani.

## ONGOZI

.....

Ni mafundisho ya Biblia kwamba viongozi wawe watu wasio na lawama na pia wawe mfano kwa Wakristo katika kila fani ya maisha yao. Wahudumu wa injili, waalimu wa shule ya Jumapili, viongozi wa uimbagi, na hata mashemasi wanahitaji kuva (njie na ndani ya kanisa) hivi kwamba wawewe kuutukuza utakatifu. Kiongozi akikosa kuishi kulingana na mafundisho hayo ya Biblia ni jambo ambalo litamfanya kuwa hafai kushikilia wadhifa na uongozi wa kanisa.

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

## SOMO: JINSI MTU WA NJE ANAVYOONEKANA

**Somo la Biblia:** *Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenywewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu. —I Wakorintho 6:19-20.*

**Muhstasari:** Watu wa Mungu wanastahili kuva mavazi ya viwango vya wastani na yenyekupeza, na waepuke kuva vito na vipodozi. Jinsi mtu anavyoonekana kwa njie inahitaji kuwa ndio mwanga wa kuangazia jinsi yeze alivyo na unyenyekevu na usafi wa ndani.

### I. Umuhimu wa Jinsi Mtu Anavyoonekana kwa Nje

- A. Samueli 16:7 Mwanadamu hutazama jinsi mtu anavyoonekana kwa njie.
- B. Mathayo 5:14-16 Nyinyi ni nuru ya ulimwengu.

### II. Mtu wa Ndani

- A. Mathayo 15:17-20 Mambo yanayomajisi mtu.
- B. Isaya 57:15 Roho iliyotubu na kunyenyeka.
- C. 1 Petro 5:5 Kuva vazizi la unyenyekevu.
- D. 1 Petro 3:4-5 Mtu aliyefichika ndani ya moyo wa mtu.

### III. Mambo ya Kwanza Yawekwe Mwanzoni

- A. Waefeso 2:8-10 Tumeokolewa kwa neema sio kwa matendo mema.
- B. Mathayo 23:25-28 Takasa kwanza kilicho ndani.

### IV. Kuitwa ili Tuwe Watakatifu

- A. Waefeso 12:14 Tafuta utakatifu.
- B. Warumi 6:22 Tunda la utakatifu.
- C. Waefeso 4:21-24 Kumvaa mtu mpya.
- D. 1 Petro 2:9 Uzao mteule, watu spesheli.

### V. Viwango vya Biblia Kuhusu Mavazi

- A. Mwanzo 3:7-10,21 Mungu alivalisha Adamu na Hawa mavazi.
- B. Isaya 47:2-3 Mifano kutoka Agano la Kale la mtu kuwa uchi.
- C. Yohana 21:7 Uchi amba Petro alikuwa nao.

- D. Kumbukumbu la Torati 22:5 Mavazi yanayofaa kuvaliwa na watu wa jinsia moja au nyininge.

- E. 1 Timotheo 2:9 Mavazi ya kiwango cha wastani, yenyekupeza kuzingatia adabu nzuri (1 Petro 3:3).

- F. 1 Timotheo 4:12 Mfano wa usafi.

### VI. Mambo ya Dunia

- A. Warumi 12:2 Msiiifuatise namna ya dunia hii.
- B. 1 Yohana 2:15-17 Msipende ulimwengu.

### VII. Vito na vipodozi

- A. 1 Timotheo 2:9-10 Mapambo yakatazwa (1 Petro 3:3).
- B. Isaya 3:16-24 Hukumu za Mungu (Yeremiah 4:30).

### VIII. Nywele

- A. 1 Wakorintho 11:14-15 Urefu wa nywele.
- B. 1 Timotheo 2:9; 1 Petro 3:3 Iliyopangwa kwa urahisi.

### IX. Viwango na Vipimo

- A. 2 Wakorintho 10:12,18 Mtu anayesifiwa na Bwana.
- B. Yohana 12:48 Kuhukumiwa na Neno la Mungu.
- C. Isaia 62:10 Inua bendera ya kuwaonyesha watu wa Mungu viwango vinavyofaa.
- D. 1 Yohana 5:3 Kumpenda Mungu.

#### **Hitimisho:**

*Kwa kuwa Bwana awaridhia watu wake; Huwapamba wenye upole kwa wokovu .*

—Zaburi 149:4

# Mavazi ya Mkristo

**Tabia za wastani:** Tabia zinazoongowa na hisia kwamba kitu kinafaa au hakifai; matendo yasiyo ya kujiweka mbele au kukosa aibu; kutokuwa na upotovu au uasherati.

Jambo linalofaa; lenye utaratibu; la viwango nya wastani; la kiasi, liisilovuka mipaka, lisilofuja mali.

**Mtu mtulivu:** Mwenye kiasi na mwenye kufuata mambo ya viwango nya katikati; bila utani mwingu; mwenye upole; asiyefanya mambo kama ya mlevi.

**Mtu mwenye soni:** Mtu mwenye kuzingatia viwango nya wastani; mwenye ucheshi na haya.



## Kuitwa Kutoka Gizani

Kwenye kizazi hiki kanisa la Mungu lingali taifa teule. Watu wa Mungu wangali wametengwa na dunia kama vile Kristo alikuwa ulimwenguni lakini hakuwa wa ulimwengu. Kila mtoto wa Mungu ni mmoja wa washirika wa "aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu" (1 Petro 2:9). Ni jukumu na wadhifa mkubwa kwa watu wa Mungu kuruhusu mwangaza wa maisha yao kung'aa ili watu wengine wauone utakatifu wa Mungu uliomo ndani yao (Mathayo 5:14-16). Ingawa makanisa mengi yameshindwa kuyadumisha mafundisho ya biblia kuhusu tabia na mavazi ya kiwango cha wastani, neno la Mungu lingali halijabadilika. Ulimwengu huu hutilia mkazo sana umuhimu wa mavazi na jinsi ambavyo mtu anaonekana. Katika ulimwengu wa sasa kuna msukumo mkubwa unaowasukuma watu kuva kulingana na mitindo ya kisasa, au kuva kwa njia ambayo mwili unaonekana u wazi. Lakini Neno la Mungu limetoa mafundisho na mwongozo kuhusiana na jinsi ambavyo Mkristo anastahili kuonekana kwa mambo yake ya nje.

## Ni kwa Nini Mavazi Ambayo Mkristo Huuwa ni Swala Muhimu?

Mavazi na vile watu wa Mungu wanavyoonekana kwa nje ni jambo muhimu kwa sababu Mungu ametoa amri ya kusema kwamba "mtukuzeni Mungu katika miili yenu" (1 Wakorintho 6:20). Watu wengine hutaja 1 Samueli 16:7 na kudai kwamba jinsi mtu anavyoonekana kwa nje sio jambo muhimu, mradi moyo wake uwe safi. Andiko hilo la 1 Samueli linasema kwamba, "wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo." Ingawa ni kweli kwamba Mungu hutazama moyo wa mwanadamu, Wakristo wameitwa ili kuwa mashahidi kwa watu ambaa hawawezi kuona mioyo ya Wakristo! Wenzako

watakuchukua kulingana na jinsi unavyoonekana kwa nje, na ukweli ni kwamba wakati mwingu jinsi mtu anavyoonekana kwa nje huwa ni dhihirisho la hali yake ya moyo, imani yake, mambo anayotilia umuhimu, na jinsi mwenyewe anavyojiona. Mavazi na jinsi mtoto wa Mungu anaonekana inahitaji kuwa ni dhihirisho la ujumbe wa unyenyekevu, usafi wa Mkristo, na utakatifu wake -- maswala ambayo ndio Mungu hutilia maanani sana. Ingawa ni kweli kwamba Wakristo hawastahili kulitukuza sana swala la mavazi ya wastani, ni kweli pia kwamba kiwango cha jinsi mtu anavyojisitiri ni jambo linalofundishwa katika Neno la Mungu; basi Wakristo hawastahili tu kuvumilia mafundisho ya mavazi mbali pia wanahitaji kuyakumbatia kwa mikono miwili.

## Katika Biblia Ni Nini Maana ya Mtu Kuwa Uchi?

Hapo mwanzo kabisa, baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, wao walitambua kwamba walikuwa wako uchi. Mara moja wakajaribu kujifunika kwa majani ya mtini halafu wakajificha kwani walitambua kwamba walikuwa uchi. Nalo jambo la kwanza kabisa ambalo Mungu alifanya lilikuwa kuwaundia mavazi ya ngozi ili kuwafunika kwa kiwango kinachofaa (Mwanzo 3:7-10,21). Basi katika Maandiko uchi sio tu swala la mtu kutovaa mavazi yoyote. Ni dhahiri kwamba katika Isaya 47:2-3 mwanamke alichukuliwa kuwa yu uchi kama mguu wake ungekuwa wazi pajani (maanake ikiwa sehemu ya mguu wake iliyomo juu ya goti ikiwa inaonekana). Hebu tumpige darubini mtume Petro alipokuwa akivua samaki. Yeye aliposikia kwamba Bwana Yesu alikuwa mahali hapo, "akajifunga vazi lake (maana alikuwa uchi), akajitupa baharini" (Yohana 21:7). *Kamusi ya Biblia ya Smith* inasema kwamba wake kwa waume wa siku hizo

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)

**Mavazi na jinsi  
mtoto wa  
Mungu  
anaonekana  
inahitaji kuwa ni  
dhihirisho la  
ujumbe wa  
unyenyekevu,  
usafi wa  
Mkristo, na  
utakatifu wake  
—maswala  
ambayo ndio  
Mungu huyatilia  
maanani.**



(Endelea kutoka ukurasa 5)

## **Kiwango cha mavazi cha mtoto wa Mungu ni kile cha kuva mavazi ya kiwango cha wastani na ya bei rahisi.**

walikuwa wakivaa vazi la ndani ambalo lilibana mwili wao na ambalo lilifanana na shati ndefu. Aina moja ya vazi hilo liliundwa bila kuwa na sehemu ya mikono na lilikuwa na urefu wa kufika kwenye magoti, ilhali aina nyingine yake ilikuwa na urefu wa kufika kwenye goti na kifundo cha mguu. Lakini pia kulikuwa na vazi lingine la nje ambalo liliundwa kwa urefu mkubwa kuliko ule wa lile la ndani. Watu walisemwa kwamba wako uchi ikiwa hawakuwa wamevaa vazi la nje. Ndiposa Petro hata ingawa hawakuwa uchi kabisa alipomwona Bwana Yesu aliharakisha kuva vazi lake la nje ili ionekana kwamba amevalia kwa kiwango kinachotosha (tazama pia 1 Samueli 19:24). Basi maandiko hayo yameanza kudhihirisha mawazo ya Mungu kuhusiana na swala la mtu kuwa yu uchi. Ulimwengu wetu umejaa watu wanaovaa suruali fupi, minisketi, na nguo zingine fupi fupi. Kwa kweli jambo hilo liko kinyume na Neno la Mungu na linavunja kanuni za Agano la Kale, kanuni ambazo hazikuwa za kiwango cha hali ya juu kama zile zinazopatikana katika Agano Jipya.

## **Tofauti Iliyopo Kati ya Jinsia Moja na Nyingine**

Kumbukumbu la Torati 22:5 inasema "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako." Hata ingawa kuna uwezekano andiko hilo lilikuwa limekusudiwa kuwakataza wanawake kuijunga jeshini, lakini pia lilitoa mwongozo kwamba kwa jumla Mungu hapendezwi wakati mambo yanayotofautisha wake kwa waume yanapotupiliwa mbali. Kusema kwamba tamaduni za kisasa zinakubali mambo mengine sio kumaanisha

kwamba Mungu anakubali mambo hayo. Aina yoyote ya nguo ambayo inavunja mipaka kati ya waume na wake ni chukizo kwa Mungu. Jamii ya sasa inafanya juu chini kuziba mipaka, sio tu kuhusiana na wajibu amba Mungu ametoa kwa wake na waume, mbali pia hata kuziba jinsi jinsia hizo zinavyoonekana. Wanawake walianza kuva suruali ndefu kwa sababu waliacha wajibu waliopewa na Mungu kama wanawake. Jambo hilo sio tu kinyume na mipango ya Mungu lakini pia ni kinyume na mpango ule mkubwa amba ulitolewa na Mungu kuhusu majukumu ambayo Mungu amewapatia wanawake na wanaume manyumbani na katika jamii. Hivyo hivyo katika siku zetu sasa tumeanza kuona wanaume wakivaa mavazi ya wanawake. Hilo jambo kamwe halifai.

## **Maagizo ya Kuva mavazi ya Kiwango cha Wastani**

Paulo alimpa Timoteo mwongozo kamili katika 1 Timoteo 2:9 ya jinsi mwanamke mtauwa anastahili kujipamba, "Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani." Andiko hili li wazi na linamaanisha yote ambayo linasema. Kiwango cha mavazi cha mtoto wa Mungu ni kile cha kuva mavazi ya kiwango cha wastani na ya bei rahisi. Lakini wengi wa Wakristo wa siku hizi hawavai mavazi ya kiwango cha wastani na hata hawaoni haya kutokana na mavazi yao. Wake kwa waume wanastahili kufunika miili kikamilifu na pia mavazi yao yanahitaji kuwa ya heshima na yasiwe ya kubana mwili sana. Lakini watu siku hizi wanafunua miili yao sana na wanavaa nguo ambazo zinawashika sana ili kudhihirisha kilicho ndani ya nguo hizo. Mambo hayastahili kuwa hivyo kati ya watu wa Mungu. Mwanamke anahitaji kuva "mavazi ya kiwango cha wastani" na kuva kile ambacho kinakubaliana na adabu njema. Minisketi au sketi ambazo hazifikii chini kwenye miguu ni moja ya mavazi ya majivuno. Nazo sketi ambazo zina mikato mirefu upande, hata zikiwa ni ndefu kiasi gani huwa zimeshonwa kwa kusudi la kuwavutia watu hpo kwenye miguu. Jambo hilo kamwe halilingani na Neno la Mungu.

Maandiko pia yamekataza mtu kuva mavazi ya bei ghali. Mkristo hastahili kuva mavazi ambayo ni ya kuisionyesha au ya kuionyesha utajiri wake. Funzo hapa ni kwamba mavazi ya mtu yanahitaji kuwa yenye urahisi na yenye heshima. "Kupamba" mwili ina maana ya kuupanga au kuwa na utaratibu unaofaa mwilini. Hii ni kumaanisha kwamba Mkristo hastahili kuwa mzembe au mvivu kuhusu jinsi ambavyo anaonekana. Watoto wa Mungu wanahitaji kuwa watu wa mipango

katika mavazi yao, watu safi na wanaojitunza vizuri.

### **Mtu Huuva Mavazi ya Kiwango cha Wastani kwa Shauku la Kutimiza Mapenzi ya Mungu**

Mitindo na aina tofauti tofauti ya mavazi huja na kupita lakini viwango vinavyowekwa na Neno la Mungu havibadilki. Mtume Paulo aliwaagiza kusanyiko la Wakristo huko Roma: "msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujuu hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:2). Mtoto wa Mungu huwa hataki kumleeta baba yake majonzi ya moyo na hufanya juu chini ili kuufikia utakatifu amba baba yake amemwitia kuhusu mavazi badala ya kufuata njia za ulimwengu. Basi mimi ninakuomba wewe Mkristo uwe macho kwa mambo ambayo ulimwengu unatilia maanani, kwa maana mambo hayo hayalingani na matakwa ya Kristo. Uovu umekidhiri sana na jamii inaendelea kuzorota. Mtoto wa Mungu anastahili kusimama wima dhidi ya roho na upumbavu wa ulimwengu wa sasa.

### **Hatuongozwi na Shauku na Tamaa za Ulimwengu**



"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata

milele" (1 Yohana 2:15-17). Lengo la mitindo mingi ya kisasa ya mavazi ni kuwawutia watu wa jinsia ile nyingine kutazama mwili wako. Sio tu wanawake lakini hata wanaume wanasukumwa sana na jamii kuvalaa kulingana na mitindo ya kisasa na kuupa mwili kipa umbele.

Ni kweli kwamba mavazi ambayo mtu huuva huadhiri jinsi anavyojihisi na kutenda. Hebu mvalishe mtoto aina tofauti ya nguo na uone jinsi atakavyofanya. Watu wazima hawako tofauti na watoto na ndiposa ni muhimu mavazi yalingane na roho aliyemo ndani ya mtu, roho ambaye anataka kumpendeza Bwana: "Mtoto awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi" (1 Timotheo 4:12). Mtoto wa Mungu anahitaji kujipamba roho wa ndani ambaye hana majivuno na ambaye atazaa matunda mazuri kila siku ya kuwapendeza hata wanadamu wenzake.

### **Mapambo na Vito**

1 Timotheo 2:9 Imewakataza Wakristo kwa uwazi kabisa wasivae dhahabu na lulu. Jambo hilo pia linatiliwa mkazo katika 1 Petro 3:3 "Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi." Nazo hukumu za Mungu zikawaangukia mabinti wa Sayuni amba walikuwa na kiburi na walitembea kwa madaha. Mabinti hao walikuwa wakivaa vito vya aina tofauti naye Mungu akatoa hukumu dhidi yao (Isaya 3:16-24). Basi katika nyakati za Agano Jipy ni kinyume na mapenzi ya Mungu mtu kuvalaa vito na mapambo ya aina tofauti tofauti – hereni, mikufu, pete, na kadhalika. Huenda mapambo hayo yasiwe ya dhahabu ama fedha lakini yawe ya "bei ya chini," lakini hio pia ni kinyume na kanuni ya Mungu kwa Mkristo kuishi maisha rahisi na ya utakatifu. Kwa kuzingatia Neno la Mungu watoto wa Mungu wanahitaji kutambua mambo ya kiroho na kuwa waangalifu wasiangukie kwenye mtego wa kusema kwamba "mambo ya mavazi hayatajwi moja kwa moja kwenye Biblia."

### **Kujirembesha na Vipodozi**

Matumizi ya vipodozi ili kufanya mwili na uso kuonekana bora zaidi kuliko hali yake halisi hakulingani na maisha matakatifu. Vipodozi

**Mtoto wa Mungu anahitaji kujipamba roho wa ndani ambaye kamwe hana majivuno na ambaye atazaa matunda mazuri kila siku ya kuwapendeza hata wanadamu wenzake.**

(Inaendelea kutoka ukurasa 8)

vinavyopakwa kwenye uso kabla ya vingine kupakwa, rangi inayopakwa kwenye midomo (lipstiki), vipodozi vya kupakwa katika mboni za juu na chini za macho, rangi inayopakwa kwenye mashavu na hata kwenye kucha; matumizi ya kucha na kope bandia; kupodoa viungo vya mikono na miguu (pedikua na manikua); michoro ya chale mwilini n.k. mambo hayo yote ni ya kidunia na hayalingani na mielekeo ya haya ambayo Mkristo anastahili kuwa nayo, na pia hayalingani na viwango vya wastani vya mavazi ambavyo Mkristo anahitaji kudumisha. Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Basi ni ombi letu kwamba Mungu atawasaidia watu wake, sio tu kuishi kulingana na ukweli huo, mbali hata pia kuwafunza watoto hasa vijana ukweli huo kwa mfano na kwa maneno.

### **Miundo ya Nywele**

Miundo ya nywele pia ni jambo ambalo linatiliwa mkazo sana. Hata ingawa watu katika sehemu mbali mbali duniani huwa na maumbile ya nywele za aina tofauti, Biblia imetoa miongozo kadha wa kadha kuhusiana na swala la nywele; "Je! Hayo maumbile yenye hayawafundishi ya kwamba mwanamume akiwa na nywele ndefu ni aibu kwake? Lakini mwanamke akiwa na nywele ndefu ni fahari kwake. Kwa sababu amepewa zile nywele ndefu ili ziwe badala ya mavazi" (1 Wakorintho 11:14-15). Mungu hupendezwa wakati watu wake wametii Neno lake na Maandiko yanasema waziwazi kwamba mwanaume adumishe nywele yake ikiwa fupi huku nywele kubwa ya mwanamke (kama jinsi Mungu alivyomuumba) ndio kifunko chake na utukufu wake.

Jinsi ambavyo mwanaume hukata nywele yake, na jinsi ambavyo mwanamke mtawu wa Mungu anavyopanga nywele yake, ni jambo ambalo linahitaji kulingana na viwango bora vya kujisitiri na urahisi wa maisha. Kama tulivyo sema hapo mbeleni, usukaji wa nywele ama kuiunganisha na kamba zingine kichwani ni mambo ambayo yamekatazwa.

### **Usimhukumu Mtu Yeyote**

Viwango vya maisha ambavyo watu wa Mungu



Tutieni, tutieni barabara;  
toeni mawe yake;  
Twekeni bendera kwa ajili ya kabilia za watu.

wanahitaji kudumisha vinahitaji kuwa bora zaidi ya zile ambazo dunia inayodidimia inadumisha.

Hatuhitaji kufanya maamuzi kulingana na yale ambayo watu wengine wanafanya mbali kwa kulingana Neno la Mungu, kwa sababu Neno la Mungu ndilo litakalotuhukumu hapo siku ya mwisho (Yohana 12:48). Kila mtoto wa Mungu anahitaji kufanya juu chini kuongozwa na Roho wa Mungu, huku akizingatia kwamba Roho wa Mungu hatawahi kwenda kinyume na Neno la Mungu. Katika siku tunazoishi, wakati ambapo watu wanasema hakuna vipimo vya lazima kwa mambo ya kiroho, "hatuthhubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenye, wala kujilinganisha nao; bali wao wenye wakijipima nafsi zao na nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao na nafsi zao, hawana akili . . . Maana mtu mwenye kukubaliwa si yeje ajisifuye, bali yeje asifiwaye na Bwana" (2 Wakorintho 10:12,18). Tunahitaji kuwa waangalifu ili tusiwhukumu watu wale wengine kama wameokoka kwa misingi ya jinsi ambavyo wanaonekana kwa nje, kwa sababu kuna watu ambao hawajawahi kusikia ukweli na mafundisho ya Kikristo kuhusiana na mavazi. Ni mapenzi ya Mungu kwamba watu wote waelewe mwangaza huu kuhusiana na mavazi ya Mkristo.

### **Jiwekee Kiwango Chako Binafsi cha Kufuata**

Ni jambo muhimu sana kwa Wakristo kujivekea viwango vya kufuata kwa mambo tofauti tofauti maishani mwao wanapofanya mambo ya kila siku.

Bila mtu kuwa na kiwango chochote

**Bila mtu kuwa na  
kiwango  
chochote  
anachodumisha  
maishani,  
mafundisho ya  
dini yanakuwa  
jambo tupu lisilo  
na maana yoyote  
katika maisha ya  
kawaida ya mtu.**

anachodumisha maishani, mafundisho ya dini yanakuwa jambo tupu lisilo na maana yoyote katika maisha ya kawaida ya mtu. Ni kweli kwamba Biblia haijatoa mwongozo wa moja kwa moja kuhusiana na urefu wa vazi la mwanamke, au urefu wa mikono ya shati la mwanaume. Lakini, kwa kuja kwamba mwanamke huwa yu uchi anapovaa vazi lenye urefu usiofikia gotini, hii ni kusema kwamba kiwango kinachokubalika ni nguo inayoficha thuluthi tatu za miguu na shati linaloziba thuluthi tatu ya mikono ya mwanaume. Mungu anahitaji kutufunulia ukweli huu sasa wakati huu wetu ili Wakristo waweze kufanyisha kazi ukweli huo maishani mwao. Hata washiriki wa kikundi cha utakatifu wamepotea njia na kuchanganyikiwa katika swala la mavazi. Je, ni nani atakubali wito na mwongozo wa Mungu ambao unapatikana katika Isaya 62:10? "Piteni, piteni, katika malango; Itengenezeni njia ya watu; Tutieni, tutieni barabara; toeni mawe yake; Twekeni bendera kwa ajili ya kabilia za watu."

#### **Furaha ya Mtu Mtiifu**

Kuna barabara ya utakatifu ambayo ina mwinuko bora kuliko njia za dhambi za ulimwengu huu. Viwango vyta utakatifu wa nje kama viliviyowekwa na Mungu ni jambo la kupendeza sana. Amri ya kudumisha viwango vyta wastani katika mavazi sio jambo la kumwingiza mtu kifungoni. Utakatifu unao-onekana kwa nje ni moja ya matunda ya moyo na maisha safi ya Mkristo. Lakini amri ikiwa peke yake inaleta kifo, lakini Roho huleta uhai na maana. Zingatia neno lifuatalo: "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito" (1 Yohana 5:3). Mkristo huwa na furaha anapokuwa mtiifu kwa Neno la Mungu. Faida anayopata mtu kwa kuwa mtiifu ni kubwa zaidi kuliko mambo yote ambayo mtu anaweza kutoa kama sadaka ya utumishi wa Mungu. Jinsi watu wa Mungu wanavyoonekana kwa nje inastahili kuwa ni kioo cha kuonyesha kwamba wao ni raia wa ufalme wa mbinguni.

– mws

## **JE, INI ASTAHILI KUVA VAZI HILI**

(Maswahili kuhusu jinsi mtu anavyoonekana mwilini)

- Je, ni kwa nini nataka kuvaa vazi hili?
- Je, vazi lenyewe linanifanya kuhisi vipi?
- Je, vazi hili limeufunika mwili wangu vizuri?
- Je, mtu anaweza kuona mwili wangu nikilivaa?
- Je, limenibana sana?
- Je, vazi hilo ni la kiwango cha wastani na ni la heshima?
- Je, ulimwengu utaona mfano gani kutoka kwanga nikilivaa?
- Je, vazi lenyewe laonyesha unyenyekevu au laonekana kuwa ni ghali?
- Je, Mungu atapendezwa na vazi hili?

# UTAMADUNI



Kuna tofauti ambazo zitazidi kudumu kati ya mavazi yanayotumiwa na watu wa nchi tofauti tofauti na vizazi tofauti tofauti. Na ingawa Biblia haijatoa mwongozo wa moja kwa moja wa ni mavazi gani yanastahili kuvaliwa na Mkristo, kuna kanuni ambayo imetolewa katika Biblia ambayo ni zaidi ya mienendo yote ya kitamaduni. Kama vazi fulani la utamaduni wa mtu liko kinyume na Neno la Mungu basi Mkristo anastahili kufuata Neno la Mungu. Mwanamke wa Marekani anaweza kuvaa sketi na blausi ilhali mwanamke wa nchi ya Malawi anaweza kuvaa nguo

inayojulikana kama chitenje (huku nao Wamaasai wa Kenya wakiva shuka na mavazi yao ya rangi nyekundu), naye mwanamke wa nchi ya Pakistani akivaa vazi liitwalo shalwaari kameezi. Mavazi hayo yote yanawenza kukubalika machoni pa Bwana mradi tu yawe yanalingana na viwango vyta wastani, yawe marefu yasiyobana mtu, na yawe ya heshima, utaratibu n.k.

Kumeshawahi kuwa (na hata sasa kutakuwa) na wakati ambapo vazi la aina fulani katika jamii litakuwa la kuwalishwa jambo fulani. Basi kulingana na ujumbe ambao unawakilishwa na vazi hilo mtoto wa Mungu anaweza kujitenga na vazi hilo kama likiwa linawakilisha ujumbe ambao haulingani na matakwa ya Mungu. Kwa mfano, ikiwa katika siku hizi zetu kuva shati la rangi ya buluu ni kuonyesha kuunga mkono kundi la kuwatetea mashoga, basi haitakuwa busara kwa mtoto wa Mungu kuvaa shati kama hilo. Basi ni muhimu kwa Wakristo kuelewa kanuni hiyo vizuri ili kusiwe kwamba baada ya miaka 40 kupita, wakati

# MASWALI na MAJIBU

## Swali: Je, Ni Sawa Mwanamke Kuva Suruali Ndefu?

Ili tuweze kujibu swali hilo hebu tuchunguze kwa kina andiko la 1 Timotheo 2:9: "Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi . . ."

Katika lugha ya Kiyunani "mavazi ya kujisitiri au mavazi ya wastani" ni "*kosmios katastole*." Nayo *Kamusi ya Vine ya Uchambuzi wa Maneno ya Agano Jipy* inasema vazi lenye kustiri, yaani *kosmios*, ni vazi la mpango, lililopangwa vizuri, lenye heshima, na lenye kudumisha viwango vya wastani. Neno hili wastani linatumika pia kuhusu heshima na tabia za mtu.

Chimbuko la neno *katastole* au vazi ni maneno mengine mawili – *kata na stole*. Neno *kata* linamaanisha sehemu ya chini, vazi linalofika chini, nalo *stole* ni vazi refu, vazi la nje lisilombana mtu sana, linalomfunika vizuri. Kulingana na *mpangilie wa maneno ya lugha ya Kiyuni katika Agano Jipy la KJV, catastole* ni neno lenye maana ya "kuangusha chini, kuiruhusu ianguke, kuruhusu vazi kufika chini; nguo, vazi alilovaa mtu."

Mchanganuzi wa maneno Adam Clark amesema yafuatayo kuhusu *katastole*:

Inaonekana kana kwamba hapa mtume anazungumza kuhusu sehemu tofauti za nguo iliyovaliwa na Wayunani na Warumi. Mbeleni nguo hiyo iliyojulikana kama *stola* ili kuwa ni nguo iliyoshonwa kwa urahisi. Yenyewe ilikuwa nguo ndefu ama vazi ambalo lilikatwa ili kichwa kiweze kuptitia kwenye mkato huo. Vazi lenyewe lilifika kwenye unyayo wa mguu, katika sehemu ya nyuma na mbele, na kushikiliwa na mshipi kuunzunguka mwili, mshipi ambaao ulipitia mbavuni. Wakati mwingine vazi hilo liliundwa kwa mikono mirefu, na wakati mwingine kwa mikono mifupi; na hata kwenye mabega yote mawili vazi hilo likashikwa kwa mshipi ili liweze kumshika mvaaji vizuri mbegani. Wanawake wengine wa Kiyunani walivaa vazi hilo huku likiwa limefunguka kila upande kutoka sehemu ya chini hadi hapi juu ya goti, ili sehemu ya paja ionekane wazi. Wanawake kama hao walijulikana kama wachambuzi wa paja; lakini ni angalau wasichana wa umri mdogo ama wasiokwu na tabia za wastani zinazokubalika ndio tu walikata vazi hilo hivyo.

Vazi la *katastole* nalo liliundwa kama lile la stola. Lenyewe liliangukia hadi kwenye sehemu ya katikati ya mwili, kwenye sehemu ya mbele na nyuma ya mwili, halafu likafungwa kwenye bega kwa mshipi au kamba, na pia lenye mkato katika sehemu ya juu ili kichwa kipitie humo, halafu likapita juu ya vazi la ndani la stola bila kubana stola . . . basi hakuna vazi la kiwango cha wastani ambalo lilishawahih kushinda hilo lilioundwa na Wayunani. Vazi kama hilo pia lilipatikana huko Uingereza hapo karibu mwaka wa 1805, na lilifanana sana na *katastole* kwa urahisi wake, heshima yake, na utukufu wake. Lakini muda si muda vazi hilo likatoweka kutoka Uingereza na badala yake mavazi ya kukosa heshima na ya kishenzi yakasambaa kote. Vazi hilo lililofanana na *katastole* lilikuwa linaambatana sana na viwango bora vya wastani vya kijamii hivi kwamba halingeweza kudumu muda mrefu. Pia lililingana sana na dini rahisi ya kweli ambayo nayo haingeweza kuendelea kuvumiliwa katika ulimwengu uliokuwa giza-giza na uliotilia mkazo sana urembo wa nje wa mtu.

Basi kiwango halisi cha Biblia cha mavazi ya mwanamke ni kwamba avae "kosmos *katastole*" – vazi la kiwango cha wastani, vazi la heshima, vazi ndefu, lisilombana na linaloteremka hadi chini. Vazi lililoshonwa kama suruali ndefu haliwezi kuambiwa kwamba ni vazi ambalo "limeruhusiwa kuanguka hadi chini," pia haliwezi kusemwa kwamba limeteremka hadi unyayoni." Hii ndio sababu suruali ndefu, minisketi, nguo fupi, nguo zinazombana mtu sana n.k. haziwezi kuchukuliwa kuwa ni nguo za kiwango cha wastani ambazo zinaweza kuvaliwa na mwanamke anayedai kuwa ni mcha Mungu.



Lakini zaidi na kuangalia Maandiko kuhusu mtu kucaa mavazi yanayomstiri vizuri, ni muhimu kwetu kuangalia swala la wanawake kucaa suruali ndefu, vazi la wanaume. Agano la Kale linafunza kwamba mwanamke asivae vazi la mwanaume (Kumbukumbu la Torati 22:5).

Kaptura zenyen urefu wa kutoka kiunoni hadi mapajani ni vazi ambalo makuhani wa Agano la Kale walilivaa (Kutoka 28:42). Kulingana na mpangilie wa maneno ya Kiebrania “kaptura” hizo zilikuwa suruali ndefu ambaa urefu wake ulifika gotini, au chini ya goti, au kwenye kiwiko cha mguu. Katika siku za Biblia wanawake hawakucaa suruali ndefu. Ni hadi hapo katika karne ya Ishaireni kwenye nchi za Ulaya ndipo wanawake walianza kucaa suruali hizo ndefu. Katika miaka ya Vita Vikuu vya Dunia, wakati ambapo wanaume walienda vitani, wanawake walitoka manyumbani mwao na kuenda kufanya kazi kwenye viwanda n.k. na wengi wao wakaanza kucaa suruali ndefu wakiwa makazini. Halafu wakati vuguvugu la kutetea haki za wanawake lilipozinduka kulianza kuwa na msukumo wa wanawake kuacha wajibu wao kama “wajenzi wa nyumba” na kuanza kushindana na wanaume makazini na kwenye jamii. Basi ikawa kwamba majukumu yaliyowekwa na Mungu kwa wanawake na kwa wanaume manyumbani na katika jamii yakaanza kutokomea. Tendo la wanawake kucaa suruali ndefu likawa ni njia moja ya vuguvugu la kutetea haki za wanawake kujieleza. Suruali ndefu ikawa ishara ya mamlaka, hii ndio sababu watu wengine huuliza swalii: “Ni nani anayevaa suruali ndefu katika nyumba hii?” Ni jambo la kusikitisha kwamba hata washirika wa kanisa la utakatifu wameadhirika sana na mitazamo ya watetezi wa haki za wanawake, mitazamo ambayo ni kinyume na mafundisho ya Maandiko.


Mungu aliwaumba wanaume na wanawake wakiwa viumbe tofauti, Yeye anatarajia wake kwa waume kutenda mambo yanayofaa jinsia yao. Lakini jamii inafanya juu chini kuvunja mipaka iliyoko kati ya waume na wake, na nguo ni moja ya mipaka hiyo. Ikiwa ishara inayopatikana mlangoni wa vyoo vya wanaume ni mchoro wa mwanaume akivaa suruali ndefu, huku ishara ya vyoo vya wanawake ikiwa ni mchoro wa mwanaamke akivaa nguo

ndefu, basi ni kusema kwamba hata ingawa ulimwengu huu unaendelea kopotoka jamii ya sasa iliyojaa dhambi ingali inatambua kwamba kuna tofutti kati ya wanawake na wanaume.

Katika utamaduni wa Nchi za Ulaya wanawake ambaa hucaa mavazi ya kiwango cha wastani huonekana kuwa ni spesheli, hata watu walioko karibu nao hutambua kuwa wao ni washiriki wa kundi la utakatifu. Basi tunahitaji kuwa makini ikiwa kama hata ulimwengu unamtambua mwanaamke anayevaa nguo ya kiwango cha wastani kama Mkristo mtakatifu.

Kwa karibu miaka 6000 wanawake walivaa nguo ndefu, wakavaa gauni n.k. Ni katika miaka 100 tu iliyopita ndipo watu wameanza kusema kwamba nguo ndefu “zinasumbua” mtu akizivaa. Pia tunahitaji kuzingatia kwamba hata katika ulimwengu huu wa sasa mwanaamke akitaka kujulikana kama mwanaamke halisi anayetambulika kwa heshima za kike yeye hucaa nguo ndefu.

Neno la Mungu halijabadilika na njia yake ingali inafaa na ni kamilifu. Ni jambo muhimu waume kwa wake kutenda mambo kama Wakristo na kutimiza wajibu ambaa Mungu amewaitia. Hata ingawa ni kinyume cha Maandiko mwanaamke kucaa suruali ndefu, kilicho chukizo zaidi ni ile roho ambayo inaleta mambo hayo. Ni ombi letu kwamba Mungu atawapatia watu wake maono na uwezo wa kuelewa ili wawe mwanga unaong’aa hadi wakati Yeye atakaporudi ulimwenguni.



—mws



**JE, WAJUA?**

**Je, mtu kuva viatu vya visigino virefu ni jambo linalokubaliana na mafundisho ya Biblia kuhusu maisha ya utakatifu, mavazi yanayolingana na kiwango cha wastani, na roho ya unyenyekevu? Hebu turuhusu ulimwenguni wenyewe kujibu swali hilo.**

Alexandra Shulman aliandika kwenye nakala aliyoita: *Ni kwa nini Mhariri wa Gazeti la Vogue daima atavaa viatu ambavyo visigino vyake vimeinuka:*



“Lakini viatu vyenye kuinua sehemu ya nyuma ya mguu . . . aha! sasa umesema. Viatu kama hivyo vyenye visigino virefu havimfanyi mtu kuonekana tu kuwa mrefu kuliko alivyo, lakini pia vinaadhiri jinsi anavyotembea na anavyojihisi . . . vinakufanya usimame wima na kujihisi kwamba u nambari moja. Na unapojihisi hivyo inakuwa rahisi wewe kufanya mambo kwa njia hiyo.”



## Kutengwa Kwa Ajili ya Injili

**Anwani**

The Gospel Truth  
605 Bishops Ct.  
Nixa, MO 65714  
USA

Email:  
[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

**UTAKATIFU KWA BWANA**

*Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu. —Warumi 1:1*

Hakuna wito mkubwa zaidi kuliko mtu kuitwa kuwa mtumishi wa Kristo. Ni heshima na mweke mkuu mtu kumtii Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, badala ya mtu kufuata mambo ya dunia. Kuwashudumia waliopotea na washiriki wa nyumba ya imani sio tu kazi ya kawaida mbali ni wito wa kiungu kutoka kwa Bwana wetu.

Roho wa Bwana angali anawaita watu wa Mungu kuhudu-mu katika injili. Hata ingawa kuna miito ya aina tofauti tofauti, Yeye angali anawatafuta wale ambao watatoa mi-ojo yao mhanga, watakaotoa wakati wao, na nguvu zao ili kuhudumu katika injili. Mtume Paulo alitengwa na kuwe-kwa wakfu ili atumikie injili ya Mungu. Yeye alipata wito wa kuacha mambo ya dunia na kujitenga ili kutimiza wito wa maisha yake yaliyobaki kwa kuhudumu katika injili. Kwa kweli kunaweza kuwa na watu ambao Bwana amewaita kutumika kwa muda katika injili, lakini Mungu hana nafasi kwa wale ambao hawako tayari kujitoe kwake kabisa. Katika kizazi hiki chetu kungali ku-na haja ya wahudumu wa injili waliojitenaga na mambo yanayowafunga ili wajitoe mhanga kwa juhudzi za kueneza injili katika nchi yao na hata katika nchi za mbali.

Kama wewe umeitwa na Mungu na kutengwa na Mungu ili kuhudumia injili, basi jipe moyo na uwe mjasiri huku ukibaki mwaminifu hata wakati una mahitaji makubwa, kwa sababu Bwana wako atakutana na mahitaji hayo yako.



—mws